

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA
KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA
KUMALIZA ELIMU YA MSINGI
MWAKA 2013**

KISWAHILI

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA
MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA
MSINGI MWAKA 2013**

KISWAHILI

Kimechapishwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2013

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI	IV
1.0 UTANGULIZI	1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA	1
2.1 SEHEMU A: SARUFI	1
2.2 SEHEMU B: LUGHA YA KIFASIHI	19
2.3 SEHEMU C: UFAHAMU	29
2.4 SEHEMU D: USHAIRI	39
2.5 SEHEMU E: UTUNGAJI	45
3.0 HITIMISHO	46
4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO	48
KIAMBATISHO A	49

DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Kiswahili imeandalisha kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakaguzi, watunga mitalaa na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya mtihani huo. Majibu ya wanafunzi katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo wanafunzi waliweza kujifunza kwa ufasaha na yale ambayo hawakuweza kujifunza kwa ufasaha katika kipindi cha miaka saba ya elimu ya msingi.

Katika taarifa hii, mambo mbalimbali ambayo yamechangia watahiniwa kushindwa kujibu maswali kwa usahihi yameainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa yafuatayo yamechangia kuwafanya wanafunzi kutoweza kujibu maswali kwa usahihi: kushindwa kutambua matakwa ya swali, kuwa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali katika somo; kutofahamu kanuni za lugha na matumizi ya misamiati; kutojibu kabisa baadhi ya maswali au kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo katika mtihani. Uchambuzi kwa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati watahiniwa walipokuwa wanajibu maswali yao zimeainishwa kwa kuonesha idadi ya watahiniwa waliojibu maswali kwa usahihi, walioshindwa kuchagua jibu sahihi, walioacha kujibu swali na ambao waliandika jibu zaidi ya moja katika swali husika.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kupata ufumbuzi wa dosari zilizoainishwa katika taarifa hii.

Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa endapo maoni yaliyotolewa yatafanyiwa kazi ipasavyo, ujuzi na maarifa watakayopata wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi vitaongezeka na hatimaye kiwango cha ufaulu katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kitaongezeka pia.

Mwisho Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, Makatibu Muhtasi na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii. Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekazo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kwa ujumla ambayo yatasaidia katika kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa siku zijazo.



Dkt. Charles E. Msonde
KAIMU KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kuhusu namna ambavyo watahiniwa walijibu maswali katika mtihani wa somo la Kiswahili. Mtihani wa Kiswahili ulikuwa na maswali **50** ya kuchagua jibu sahihi ambayo yalikuwa yamegawanywa katika sehemu tano kama ifuatavyo: Sehemu A: Sarufi; B: Lughya ya Kifasihi; C: Ufahamu; D: Ushairi; na E: Utungaji. Jumla ya watahiniwa **867,983** walisajiliwa kufanya mtihani wa **PSLE 2013** ambapo miongoni mwao waliofanya mtihani wa somo la Kiswahili walikuwa **844,719** na katika yao watahiniwa **583,348** sawa na asilimia **69.06** walifaulu mtihani huo.

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa kwa kila swali umefanyika na sehemu hii inaanisha maswali yaliyoulizwa na majibu ya kuchagua waliyopewa. Idadi ya watahiniwa waliochagua kila jibu na asilimia yao imeoneshwa. Aidha uchambuzi wa sababu zinazoweza kuwa zilichangia kuwafanya wasichague jibu sahihi zimeainishwa.

2.1 Sehemu A: Sarufi

Swali la 1: Sweta langu limeshonwa na fundi mzoefu? “Mzoefu” ni aina gani ya neno?

- A. Kielezi
- B. Kivumishi
- C. Kiunganishi
- D. Nomino
- E. Kitenzi.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B*	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	275,841	317,788	77,172	111,598	57,810	2,226	2,318
Asilimia ya watahiniwa	32.65	37.62	9.14	13.21	6.84	0.26	0.27

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua aina za maneno. Asilimia 37.62 ya watahiniwa walichagua jibu B “Kivumishi” ambalo ndilo jibu sahihi. Asilimia 32.65 ya watahiniwa walichagua kipotoshi A ambacho ni kielezi. Watahiniwa hao walipotoshwa na kitenzi “limeshonwa” ambacho kilifuatwa na “fundi mzoefu,” hivyo kuona jibu sahihi ni kielezi na kusahau kuwa neno fundi ni nomino. Hata hivyo, kwa kanuni ya lugha ya Kiswahili nomino haiwezi kufuatwa na kielezi. Hali kadhalika kuwepo kwa asilimia 9.14 ya watahiniwa waliochagua kipotoshi C “Kiunganishi” inaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kujua kuwa neno “mzoefu” sio kiunganishi kwa sababu kwa kuzingatia sintaksia ya lugha ya Kiswahili neno ambalo ni kiunganishi haliwezi kukaa mwishoni mwa sentensi. Asilimia 13.21 ya watahiniwa walichagua kipotoshi D “Nomino” ambacho ni jina linalosimamiwa na neno “fundi” na wala sio kivumishi na asilimia 6.84 walichagua E “Kitenzi” ambacho nacho hakitoi taarifa yoyote kuhusu kazi ya Nomino.

Swali la 2: “Ningejua ukweli wa mambo kabla _____ hapa bure saa hizi.” Neno gani linakamilisha sentensi hiyo?

- A. nisingalikuja
- B. ningekuja
- C. singelikuja
- D. nisingelikuja
- E. nisingekuja.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D	E*	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	56,299	211,534	58,302	131,989	382,461	1,839	2,329
Asilimia ya watahiniwa	6.66	25.04	6.9	15.62	45.27	0.22	0.28

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kutumia maneno katika sentensi zenyenye masharti. Watahiniwa walio wengi walikuwa na uelewa wa swali hili kwani asilimia 45.27 walichagua jibu E ambalo ni sahihi. Uchaguzi wa kipotoshi B “ningekuja” kwa watahiniwa 211,534 ambao ni sawa na asilimia 25.04 unaonesha kuwa watahiniwa hao waliathiriwa na umbo la “nge” ambalo pia linajitokeza katika kitenzi “Ningekuja” bila kuzingatia taratibu kuwa kauli hiyo ni ya kujilaumu yaani “ningejua” hivyo hukamilishwa na ukashindwa kufuata masharti ya umbo la “nge” kufuatiwa na umbo la “nge.”

Swali la 3: “UKIMWI unaua.” Mbunge alisema. Ipi ni kauli taarifa ya sentensi hiyo kati ya hizi zifuatazo?

- A. Mbunge aliwaambia UKIMWI unaua
- B. Mbunge alisema UKIMWI unaua
- C. UKIMWI unaua mbunge alisema
- D. Mbunge alisema kwamba UKIMWI unaua
- E. Mbunge alieleza UKIMWI unaua.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D*	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	86,702	216,379	96,050	394,268	46,404	2,427	2,523
Asilimia ya watahiniwa	10.26	25.61	11.37	46.67	5.49	0.29	0.3

Swali lililenga kupima ujuzi wa watahiniwa katika kuelewa kauli za sentensi na lilitaka mtahiniwa kuonesha sentensi aliyopewa ipo katika kauli gani? Aslimia 46.67 ya watahiniwa walichagua jibu D “Mbunge alisema kwamba UKIMWI unaua” ambalo ni jibu sahihi. Uchaguzi huu unaonesha kuwa watahiniwa walielewa kuwa kauli taarifa inaambatana na neno “kwamba” katika kueleza kile kilichosemwa. Kuwepo kwa jumla ya asilimia 52.73 ya waliochagua kati ya vipotoshi A, B, C na E kunaonesha wazi kuwa watahiniwa walikosa ujuzi unaotawala muundo wa kauli katika sentensi. Hivyo watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa umbo la “kwamba” lilikuwa kigezo muhimu katika kutoa kauli ya taarifa.

Swali la 4: “Anna anatembea polepole _____ twiga.” Kifungu kipi cha maneno kinakamilisha sentensi hiyo?

- A. mithili ya
- B. mathalani ya
- C. mahadhi ya
- D. maridhawa ya
- E. madhali ya.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A*	B	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	422,895	117,383	80,359	126,784	89,662	4,730	2,940
Asilimia ya watahiniwa	50.06	13.9	9.51	15.01	10.61	0.56	0.35

Swali lililenga kupima matumizi ya msamiati wa Kiswahili ambapo ni asilimia 50.06 ya watahiniwa ndio waliochagua jibu A “mithili ya” ambalo ndilo jibu sahihi. Asilimia 15.01 walichagua jibu D “maridhawa ya” ambalo si jibu sahihi kwani neno hilo maana yake ni kuridhisha. Aidha, uchaguzi wa kipotoshi B “mathalani ya” kwa asilimia 13.9 ambalo sio jibu sahihi inaonesha kuwa watahiniwa walipotoshwa na neno “mathalani” ambalo lina maana ya mfano lakini walishindwa kuelewa kuwa kisarufi mathalani haiendani na “ya”. Uteuzi wa vipotoshi C “mahadhi ya” na E “madhali ya” unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa maana mbalimbali za maneno kwani kila kifungu cha maneno kilikuwa na maana tofauti kabisa na kingine. Aidha mahadhi yanahuisha upandaji na ushukaji wa sauti katika uimbaji na “madhali ya” ikiwa na maana ya “kwa sababu,” hivyo vifungu vyote vina maana tofauti na “mithili ya.”

Swali la 5: Neno lipi halilandani na maneno yafuatayo?

- A. Msonge
- B. Tembe
- C. Daraja
- D. Kibanda
- E. Ghorofa.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C*	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	117,640	182,789	399,380	51,234	87,293	3,507	2,910
Asilimia ya watahiniwa	13.93	21.64	47.28	6.06	10.33	0.42	0.34

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutumia msamiati. Ni asilimia 47.28 ya watahiniwa waliofanya mtihani waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni C “Daraja.” Asilimia 21.64 ya watahiniwa walichagua B “Tembe” ambalo si jibu sahihi. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa maana ya neno “Tembe” ambalo ni aina ya nyumba inayotumiwa na aina mbalimbali ya makabila hapa nchini. Aidha, uchaguzi wa vipotoshi A, D na E kwa asilimia 30.32 ambavyo vyote pia ni majina ya aina mbalimbali za nyumba, unaonesha kuwa hawana maarifa ya kutosha ya misamiati ya lugha ya Kiswahili. Hivyo watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa vipotoshi hivyo vinne ambavyo havikuwa majibu sahihi vyote vilikuwa na maana moja ambayo ni aina za nyumba.

Swali la 6: Sentensi ipi kati ya hizi zifuatazo ni kauli ya kutendea?

- A. Watoto wanacheza mpira
- B. Mpira unachezwa na watoto
- C. Watoto wanachezeana mpira
- D. Watoto wanachezea mpira
- E. Mpira unachezewa na watoto.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D*	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	152,787	133,451	94,744	337,812	119,710	3,191	3,058
Asilimia ya watahiniwa	18.09	15.8	11.22	39.99	14.17	0.38	0.36

Swali lililenga kupima ujuzi wa kauli za vitenzi. Asilimia 39.99 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi D “Watoto wanachezea mpira.” Sababu iliyowafanya watahiniwa kupata swali hili kwa usahihi ni uwezo wa kuhusisha umbo la kisarufi -e- liliopo katika kauli ya kutendea na umbo -e- liliopo katika kitensi “wanachezea.” Watahiniwa waliochagua kati ya vipotoshi A, B na E amba ni asilimia 48.06 walishindwa kugundua upungufu uliokuwepo katika vipotoshi hivyo ambapo umbo -e- halionekani likijipambanua. Aidha waliochagua kipotoshi C amba ni asilimia 11.22 walivutiwa na umbo la -ean- bila kujuua kuwa umbo hili lipo katika kauli ya kutendeana na wala sio kutendea.

Swali Ia 7: “Tumejifunza _____ kujikinga na VVU na UKIMWI.” Kifungu kipi cha maneno kati ya vifuatavyo kinakamilisha sentensi hiyo?

- A. ibara ya
- B. jinsi ya
- C. jinsia ya
- D. ilhali ya
- E. aina ya

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B*	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	32,111	656,931	66,338	28,572	56,135	1,962	2,704
Asilimia ya watahiniwa	3.8	77.77	7.85	3.38	6.65	0.23	0.32

Swali lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kutumia sarufi ya lugha. Swali hili ni mionganoni mwa maswali yaliyojibwa kwa usahihi na idadi kubwa ya watahiniwa katika mtihani huu ambapo 77.77 ya watahiniwa ndio waliochagua jibu sahihi yaani B “jinsi ya.” Uchaguzi wa kipotoshi C “jinsia ya” unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa kuelewa tofauti iliyopo kati ya “jinsi ya” ikiwa na maana “namna ya” na “jinsia ya” maana yake ikiwa ni hali ya kuwa mume au mke. Aidha uchaguzi wa vipotoshi A “ibara ya” D “ilhali ya” na E “aina ya” kwa asilimia 13.83 unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuelewa maana ya maneno hayo na jinsi yasivyoweza kuikamilisha sentensi iliyotolewa.

Swali la 8: Sehemu ambayo ng’ombe huogeshwa ili kuwaepusha na magonjwa huitwaje?

- A. Mto
- B. Bwawa
- C. Ziwani
- D. Josho
- E. Joshi.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D*	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	70,687	87,495	55,231	416,752	208,026	3,515	3,047
Asilimia ya watahiniwa	8.37	10.36	6.54	49.33	24.63	0.42	0.36

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiazi unaoonesha uhusiano wa sehemu mbalimbali ambapo huwepo maji au chombo kinachohusika na maji. Asilimia 49.33 ya watahiniwa walichagua jibu D “Josho” ambalo ni jibu sahihi. Uchaguzi wa vipotoshi A, B na C kwa

asilimia 25.27 ulidhihirisha kuwa baadhi ya watahiniwa walikuwa hawajui msamiati sahihi unaoelezea sehemu inayotumika kuwaogeshea ng'ombe ili kuwaepusha na magonjwa kwani Mto, Bwawa na Ziwani ni sehemu zenyе maji na huenda ng'ombe wangeweza kuogeshewa lakini hazina dawa maalum kwa ajili ya kuwaogesha na kuwaepusha na magonjwa. Uchaguzi wa kipotoshi E "Joshi" ambacho sio jibu sahihi kikiwa na maana ya sehemu ya mbele au tanga la mbele la chombo kinachosafiri ndani ya maji ultokana na kuvutiwa tu kwa watahiniwa kutokana na athari za kimatamshi.

Swali la 9: "Mboga haina chumvi ya kutosha." Wingi wa sentensi hiyo ni upi?

- A. Mboga hazina chumvi ya kutosha
- B. Mboga haina machumvi ya kutosha
- C. Mamboga hayana chumvi ya kutosha
- D. Mamboga hayana chumvi za kutosha
- E. Mboga haina chumvi za kutosha.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A*	B	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	571,409	54,177	55,294	50,746	107,616	2,653	2,858
Asilimia ya watahiniwa	67.64	6.41	6.55	6.01	12.74	0.31	0.34

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutumia maneno katika umoja na wingi. Watahiniwa wengi yaani asilimia 67.64 walikuwa na uelewa wa swali hili kwani walichagua jibu A "Mboga hazina chumvi ya kutosha" ambalo ni sahihi. Uchaguzi wa kipotoshi B, C na D kwa watahiniwa 160,217 ambao ni sawa na asilimia 18.97 unaonesha kuwa watahiniwa hao waliathiriwa na tabia ya baadhi ya nomino ambazo zina uwezo wa kupokea umbo la wingi kwa mfano boga (umoja) na maboga (wingi). Hivyo kwa athari

hiyo wakaviona vipotoshi venye maneno “Mamboga” na “machumvi” kuwa jibu sahihi wakati maneno hayo hayana umoja na wingi. Uteuzi wa kipotoshi E unaonesha jinsi watahiniwa hao 107,616 sawa na asilimia 12.74 wasivyokuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu wingi wa nomino “Chumvi” ambao unabakia kuwa “chumvi” kwa umoja na wingi. Hali hii inadhihirisha kuwa watahiniwa wengi hudhani kuwa ni lazima kila nomino kuwa na umbo mahususi lioneshalo wingi.

Swali la 10: Nywele zinazoota kuanzia karibu na masikio mpaka kwenye mashavu huitwaje?

- A. Mvi
- B. Sharafa
- C. Ndevu
- D. Sharubu
- E. Kope.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B*	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	41,959	272,066	260,189	227,862	37,189	2,664	2,824
Asilimia ya watahiniwa	4.97	32.21	30.8	26.97	4.4	0.32	0.33

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutumia msamiati. Ni asilimia 32.21 tu ya watahiniwa waliofanya mtihani walioweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni B “Sharafa.” Asilimia 30.8 ya watahiniwa walichagua C “ndevu” ambalo si jibu sahihi. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa maana ya neno “ndevu” kuwa ni nywele zinazoota katika kidevu. Aidha, inawezekana watahiniwa hawakuelewa kuwa nywele zinazoanzia kwenye masikio zina jina tofauti ambalo ni sharafa. Kwa ujumla majibu yaliyotolewa na watahiniwa yanaonesha wazi kuwa hawakuwa na ujuzi wa kutosha wa

msamiati wa Kiswahili kwa vile vipotoshi A, D na E vina maana tofauti kabisa na jibu sahihi ambalo ni “Sharafa” pamoja na kwamba zote ni nywele lakini huota sehemu tofauti.

Swali la 11: Sentensi ipi kati ya hizi ipo katika hali timilifu?

- A. Mheshimiwa Rais anahutubia mukutano
- B. Mheshimiwa Rais alihutubia mukutano
- C. Mheshimiwa Rais atahutubia mukutano
- D. Mheshimiwa Rais amehutubia mukutano
- E. Mheshimiwa Rais alikuwa anahutubia mukutano.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D*	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	299,649	88,311	66,092	241,306	142,887	3,293	3,215
Asilimia ya watahiniwa	35.47	10.45	7.82	28.57	16.91	0.39	0.38

Swali lilengwa kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutumia njeo ya wakati. Asilimia 28.57 walichagua D “Mheshimiwa Rais amehutubia mukutano” ambalo ni jibu sahihi kwa kuwa kitenzi “amehetubia” kina umbo “-me-” ambalo ni umbo la hali timilifu. Asilimia 35.47 ya watahiniwa walichagua kipotoshi A “anahutubia” ambacho sio jibu sahihi kwa sababu walishindwa kutambua kuwa kitenzi hicho kina umbo “na” ambalo ni umbo la wakati uliopo hali ya kuendelea na wala sio jibu sahihi kwa sababu walishindwa kutambua maumbo yanayowakilisha dhana mbalimbali za njeo katika sarufi ya Kiswahili.

Swali la 12: Neno lipi ni **tofauti** na maneno mengine kati ya yafuatayo?

- A. Maji
- B. Maziwa
- C. Soda
- D. Juisi
- E. Samli.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D	E*	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	88,955	78,139	38,787	28,707	604,472	2,327	3,366
Asilimia ya watahiniwa	10.53	9.25	4.59	3.4	71.56	0.28	0.4

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiai unaoonesha uhusiano wa vitu vinavyotumiwa na jamii. Swali hili ni mionganii mwa maswali yaliyojibwa kwa usahihi na watahiniwa wengi kwani asilimia 71.56 ya watahiniwa walichagua jibu E “Samli” ambalo ni jibu sahihi. Uchaguzi wa vipotoshi A, B, C na D kwa watahiniwa 234,588 sawa na asilimia 27.77 ulidhihirisha kuwa watahiniwa hao walikuwa hawajui kuwa vipotoshi hivyo vina mfanano kwa kuwa maji, maziwa, soda na juisi vyote ni vinywaji lakini samli ni mafuta.

Swali la 13: “Kitabu chako ni kizuri, ukienda dukani nami uninunulie _____.” Ni kifungu kipi cha maneno hukamilisha sentensi hiyo.

- A. kama hivyo
- B. kama hiko
- C. kama icho
- D. mfano wa iko

E. kama hicho.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D	E*	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	40,158	79,487	133,888	36,987	548,722	2,455	3,056
Asilimia ya watahiniwa	4.75	9.41	15.85	4.38	64.96	0.29	0.36

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika sarufi ya lugha. Asilimia 64.96 ya watahiniwa walichagua E “kama hicho” ambalo ni jibu sahihi. Uchaguzi wa vipotoshi A, B, C na D kwa watahiniwa 290,520 ambaao ni sawa na asilimia 34.39 unadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu muundo wa sentensi katika kuangalia upatanisho wa kisarufi.

Swali la 14: “Tunda huachwa mpaka likauke.” Sentensi hiyo ikiwa katika hali ya ukarusha itakuwa ipi kati ya zifuatazo?

- A. Tunda haliachwi mpaka likauke
- B. Tunda haliachi mpaka likauke
- C. Tunda halikuachwa mpaka likauke
- D. Tunda halitaachwa mpaka likauke
- E. Tunda halijaachwa mpaka likauke.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A*	B	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	471,327	63,801	100,445	145,850	57,034	3,408	2,888
Asilimia ya watahiniwa	55.79	7.55	11.89	17.27	6.75	0.4	0.34

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutambua hali mbalimbali zinazojitokeza katika sentensi. Asilimia 55.79 ya watahiniwa walichagua jibu A “Tunda haliachwi mpaka likauke” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 145,850 sawa na asilimia 17.27 walichagua kipotoshi D “Tunda halitaachwa mpaka likauke” ambacho si jibu sahihi na huenda walifanya hivyo kwa sababu walidhani kuwa ili kuonesha hali ya ukarusha ni lazima iwe katika wakati ujao jambo ambalo sio sahihi. Uteuzi wa vipotoshi B, C na E kwa asilimia 26.19 inaonesha wazi kuwa watahiniwa husika hawakuwa na ujizi wa hali mbalimbali zinazojitokeza katika sentensi. Aidha, watahiniwa hao hawakuweza kuona kuwa sentensi “Tunda huachwa mpaka likauke” ilikuwa katika wakati wa mazoea hivyo hata jibu sahihi hupaswa kuwa katika wakati huo huo wa mazoea.

Swali la 15: Mkutano haukufanyika kwa sababu mwenyekiti na katibu hawakufika. Kifungu kipi cha maneno kati ya vifuatavyo kinasadifu sentensi hiyo?

- A. Mkutano uliairisha
- B. Mkutano ulahirishwa
- C. Mkutano ulihairishwa
- D. Mkutano uliharishwa
- E. Mkutano ulihairisha.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B*	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	111,847	370,963	258,799	52,724	44,562	3,126	2,732
Asilimia ya watahiniwa	13.24	43.91	30.64	6.24	5.28	0.37	0.32

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika utumizi wa lugha. Watahiniwa 370,963 sawa na asilimia 43.91 walichagua B “Mkutano ulahirishwa” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 311,523, sawa na asilimia 36.88 walichagua kati ya kipotoshi C “Mkutano ulahirishwa” na kipotoshi D “Mkutano ulahirishwa” ambavyo sio majibu sahihi jambo linaloonesha kuwa walikosa maarifa ya semantiki ya Kiswahili. Watahiniwa hao walivutiwa na neno “hairishwa” na “harishwa” bila kutambua kuwa kisarufi hayakuwa maneno sahihi. Athari za kimatamshi zinaweza pia kuwa zilichangia kwa watahiniwa waliochagua kipotoshi A “ulairishwa” na E “Ulihairisha” badala ya “Ulahirishwa.”

Swali la 16: Mlinzi wa mlangoni huitwaje?

- A. Boharia
- B. Baharia
- C. Bawaba
- D. Banati
- E. Bawabu.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D	E*	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	103,861	139,911	311,664	116,491	164,282	5,789	2,755
Asilimia ya watahiniwa	12.29	16.56	36.89	13.79	19.45	0.69	0.33

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutumia msamiati. Asilimia 19.45 tu ya watahiniwa waliofanya mtihani walichagua jibu E “Bawabu” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 311,664 ambao ni sawa na asilimia 36.89 walichagua kipotoshi C “Bawaba” hali inayoonesha kuwa walikosa maarifa ya kuelewa maana ya bawaba kwamba ni kipande cha chuma

kinachopigiliwa kwenye mlango au dirisha ili kuwezesha kufunga na kufungua. Watahiniwa hawa walichanganya bawaba na bawabu kwa vile ni maneno yanayokaribiana kimatamshi ijapokuwa yana matumizi tofauti. Uchaguzi wa vipotoshi A, B na D kwa watahiniwa 360,263 ambaao ni sawa na asilimia 42.64 unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuelewa maana ya maneno hayo kwa vile “Baharia” ni mfanyakazi wa chombo cha baharini, “Boharia” ni mtunza vifaa katika ghala au bohari na “banati” ni mabinti au wasichana. Hivyo hii inadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa kuelewa maana ya maneno hayo.

Swali la 17: Joshua yuko jikoni anapaa samaki. Neno “anapaa” kama lilivyotumika katika sentensi hii lina maana ipi?

- A. Kuwapaka samaki chumvi
- B. Kuondoa magamba ya samaki
- C. Kuondoa mifupa katika samaki
- D. Kukausha samaki kwa moto
- E. Kuwakata samaki vipande vipande.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B*	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	78,395	394,909	45,588	274,397	46,572	2,340	2,552
Asilimia ya watahiniwa	9.28	46.75	5.4	32.48	5.51	0.28	0.3

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati. Asilimia 46.75 walichagua jibu B “Kuondoa magamba ya samaki” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 274,397 ambaao ni sawa na asilimia 32.48 walichagua kipotoshi D “Kukausha samaki kwa moto” ambacho sio jibu sahihi. Watahiniwa hao walichanganya maana ya neno ‘Kupaa’ ya kuchukua

makaa mekoni kama vile kupalia mkaa, wakalifananisha na ‘kukausha’ ambalo sio jibu sahihi. Uteuzi wa vipotoshi A, C na E kwa asilimia 20.19 ambavyo vilikuwa sio majibu sahihi viliwashawishi watahiniwa kutokana na zile hatua mbalimbali ambazo samaki huzipitia wakati wa kumtayarisha kwa kupikwa.

Swali la 18: “Mtoto wa ng’ombe anaitwa ndama, watoto wa kuku, bata, kanga wanaitwa vifaranga, kimatu ni mtoto wa nani?

- A. Nzige
- B. Nyuki
- C. Inzi
- D. Kipepeo
- E. Buibui.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A*	B	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	470,470	109,924	61,338	77,125	119,297	4,072	2,527
Asilimia ya watahiniwa	55.69	13.01	7.26	9.13	14.12	0.48	0.3

Swali lililenga katika kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua makundi mbalimbali ya nomino. Asilimia 58.89 ya watahiniwa walichagua A “Nzige” ambalo ndilo jibu sahihi. Uteuzi wa vipotoshi B, C, D na E kwa watahiniwa 367,684 sawa na asilimia 43.52 ulionesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa kuhusu nomino za viumbe mbalimbali hivyo kushindwa kujua “kimatu” ni mtoto wa nani. Aidha watahiniwa 4,072 hawakujibu swali hili.

Swali la 19: Kisawe cha neno “eupe” ni kipi?

- A. Chokaa
- B. Angavu

- C. Theluji
- D. Ukungu
- E. Angaza

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B*	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	184,999	242,924	153,338	104,114	152,024	4,688	2,666
Asilimia ya watahiniwa	21.9	28.76	18.15	12.32	18	0.55	0.32

Swali lilibenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu visawe vyta maneno. Asilimia 28.76 ya watahiniwa walichagua jibu B “Angavu” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 184,999 sawa na asilimia 21.9 walichagua kipotoshi A “Chokaa” ambalo sio sahihi kwani kila eupe sio unga mweupe ambao hupatikana kwa kuchoma mawe, hali inayoashiria kuwa ama hawakuelewa matakwa ya swali au hawakuwa na uelewa unaotakiwa wa visawe sahihi vyta maneno. Uchaguzi wa vipotoshi C, D na E ulidhihirisha pia kuwa baadhi ya watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa visawe sahihi vyta maneno. Aidha watahiniwa hao walishindwa kuelewa maana ya neno ‘eupe’ ili kuweza kupata kisawe sahihi.

Swali la 20: Siku ya nne baada ya leo huitwaje?

- A. Mtondo
- B. Mtondo kutwa
- C. Mtondogoo
- D. Kesho kutwa
- E. Mtondogoo kutwa.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C*	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	104,410	66,577	412,314	174,084	81,272	2,893	3,203
Asilimia ya watahiniwa	12.36	7.88	48.81	20.61	9.62	0.34	0.38

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutambua majina ya siku. Asilimia 48.81 ya watahiniwa waliofanya mtihani walichagua jibu C “Mtondogoo” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 278,494 sawa na asilimia 32.97 walichagua kipotoshi A “Mtundo” na D “Kesho kutwa,” Watahiniwa hao walikosa uelewa kwamba “mtondo” ni siku ya tatu na “kesho kutwa” ni siku ya pili baada ya leo. Uchaguzi wa vipotoshi B “Mtundo kutwa” na E “Mtondogoo kutwa” kwa watahiniwa 147,849 amba ni sawa na asilimia 17.50 inaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa hakuna siku zenyet kuitwa majina hayo.

2.2 Sehemu B: Lughya ya Kifasihi

Swali la 21: Tegua kitendawili kisemacho; “Mwenye kuitwa amefika lakinimjumbe bado hajarudi.”

- A. Nazi na mkwezi
- B. Yai na kifaranga
- C. Birika na chai
- D. Nyama na ngozi
- E. Chupa na mfuniko.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A*	B	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	531,352	151,088	67,837	45,568	42,330	3,583	2,995
Asilimia ya watahiniwa	62.9	17.89	8.03	5.39	5.01	0.42	0.35

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu tanzu za semi na hasa vitendawili. Asilimia 62.9 ya watahiniwa waliofanya mtihani walichagua jibu A “Nazi na mkwezi” ambalo ndilo jibu sahihi. Asilimia 17.89 ya watahiniwa walichagua kipotoshi B “Yai na kifaranga” ambalo sio jibu sahihi kwani walishindwa kuelewa kuwa vyote viwili viko sehemu moja na hakuna safari yoyote ioneshayo kuwa yupo mmoja wao anayetangulia. Uteuzi wa vipotoshi C “Birika na Chai,” D “Nyama na ngozi” na E “Chupa na mfuniko” vyote vinaonekana kuwepo pamoja na kutegemeana kwa vile kimoja hakiwezi kuwepo na kingine kisiwepo kabisa. Hii inaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa utegemezi huo.

Swali la 22: “Wakoloni walitunyanyasa lakini hatimaye unyanyasaji huo ulifika ukingoni kwani _____.” Ni methali ipi kati ya zifuatazo inakamilisha sentensi hiyo?

- A. hakuna marefu yasiyokuwa na ncha
- B. mchumia juani hulia kivulini
- C. ukiona vyaelea vimeundwa
- D. umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
- E. bandu bandu humaliza gogo.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A*	B	C	D*	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	485,482	108,277	63,433	126,139	55,445	2,801	3,176
Asilimia ya watahiniwa	57.47	12.82	7.51	14.93	6.56	0.33	0.38

Swali lilenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu methali na hasa ukamilishaji wake. Ni asilimia 57.47 ya watahiniwa waliofanya mtihani wa Kiswahili ndio waliochagua A “hakuna marefu yasiyokuwa na ncha” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 108,277 sawa na asilimia 12.82 walichagua kipotoshi B “mchumia juani hulia kivulini” ambalo sio jibu sahihi. Inawezekana watahiniwa hao walichagua jibu hilo kwa kuhusianisha swali na dhana ya faraja aipatayo mtu baada ya mateso makubwa. Aidha watahiniwa 245,017 amba ni sawa na asilimia 29.00 walichagua vipotoshi C, “ukiona vyaelea vimeundwa” D “umoja ni nguvu utengano ni udhaifu” na E “bandu bandu humaliza gogo” ambavyo vyote havikuwa majibu sahihi kwa vile vinaelezea matokeo mazuri yanayotokana na kazi ya pamoja na ushirikiano. Hivyo watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa methali waliyoulizwa ilikuwa inaonesha kuwa hakuna jambo lisilokuwa na mwisho wake bila ya kutaka kujua huo mwisho ulikuwaje.

Swali la 23: “Kidagaa kimemwozea.” Msemo huu una maana gani?

- A. Kukwepa kulipa deni
- B. Kutowajibika kulipa
- C. Kuelemewa na jambo
- D. Kupoteza tumaini
- E. Kulipa deni maradufu.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C*	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	192,645	91,149	368,544	99,386	84,901	5,040	3,088
Asilimia ya watahiniwa	22.8	10.79	43.63	11.77	10.05	0.6	0.37

Swali lililenga katika kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya misemo mbalimbali ya Kiswahili. Asilimia 43.63 ya watahiniwa walichagua jibu C “kuelemewa na jambo” ambalo ndilo jibu sahihi. Uchaguzi wa vipotoshi A, B na E kwa watahiniwa 368,695 sawa na asilimia 43.64 unadhihirisha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa maneno “kukwepa kulipa deni” ambalo lina maana sawa na “kutokuwajibika kulipa” na “kulipa deni maradufu” ikiwa na maana kulipa zaidi ya ilivyotakiwa sio majibu sahihi ambayo yangetuwa na maana ya “kidagaa kimemwozea.” Aidha uteuzi wa kipotoshi D “Kupoteza tumaini” kwa watahiniwa 99,386 sawa na asilimia 11.77 ikiwa na maana kutokufanikiwa inaonesha wazi kuwa haina maana iliyokusudiwa katika msemo huo. Hivyo uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa hawakuweza kutambua kuwa maneno yote hayo yaliyowekwa kwenye vipotoshi yana maana tofauti kabisa na ile ya msemo “kidagaa kimemwozea” ambao maana yake ni kuelemewa na jambo.

Swali la 24: “Kukubali kwa ulimi” ni msemo wenye maana ipi?

- A. Kukubali kwa dhati
- B. Kukubali kwa maneno
- C. Kukubali bila kusema neno
- D. Kukubali kimoyomoyo
- E. Kukubali kwa moyo mmoja.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B*	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	79,597	410,027	102,204	114,055	132,241	3,448	3,181
Asilimia ya watahiniwa	9.42	48.54	12.1	13.5	15.65	0.41	0.38

Swali lililenga katika kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya misemo mbalimbali ya Kiswahili. Asilimia 48.54 ya watahiniwa walichagua jibu B “kukubali kwa maneno” ambalo ndilo jibu sahihi. Uchaguzi wa vipotoshi A, C, D na E kwa watahiniwa 428,097 sawa na asilimia 50.67 unadhihirisha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa kukubali kwa dhati ina maana sawa na kukubali kwa kusema neno na hata kukubali kimoyomoyo. Uchambuzi unaonesha kuwa vipotoshi hivyo vinne vina mfanano kimaana tofauti na matakwa ya swali ambayo yanahitaji kukubali kwa ulimi tu ambayo maana yake ni kukubali tu lakini utekelezaji wa jambo haufanyiki kabisa.

Swali la 25: Nahau isemayo, “amevimba kichwa” ina maana ipi?

- A. Kupata mafanikio makubwa
- B. Kukabidhiwa madaraka ya juu
- C. Kuwa na hali ya hasira
- D. Kuwa na hali ya huzuni
- E. Kuwa na tabia ya majivuno.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D	E*	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	164,129	155,108	220,617	84,378	213,460	3,739	3,322
Asilimia ya watahiniwa	19.43	18.36	26.12	9.99	25.27	0.44	0.39

Swali lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kuhusu matumizi ya semi katika lugha ya Kiswahili. Asilimia 25.27 ya watahiniwa walichagua jibu E “kuwa na tabia ya majivuno” ambalo ni jibu sahihi. Uteuzi wa vipotoshi kati ya A, B, C na D kwa asilimia 73.9 unaonesha ni kwa kwa kiasi gani watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu semi mbalimbali za Kiswahili. Kwa mfano “kupata mafanikio makubwa” msemo unaoendana na hali hiyo ni “Kula uhondo kunataka matendo,” “Kukabidhiwa madaraka makubwa” nao huweza kuendana na nahau isemayo “Kuua tembo kwa ubua” yaani kufanikiwa jambo kwa urahisi bila ya kutarajia. Vipotoshi vingine kama “Kuwa na hali ya hasira au hali ya huzuni” vina mfanano uoneshao kuwa mtu hana raha, hivyo vyote hivyo visingefaa kuwa jibu sahihi la nahau “amevimba kichwa” ambayo maana yake ni kuwa na majivuno.

Swali la 26: “Kitanda usichokilalia hujui kunguni wake.” Methali ipi kati ya zifuatazo ina maana sawa na hiyo?

- A. Pema usipopema ukipema si pema tena
- B. Kizuri hakikosi ila
- C. Mtu siri kusema na moyo wake
- D. Nyumba usiyoilala ndani hujui ila yake
- E. Pilipili usiyoila yakuwashia nini.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D*	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	96,096	80,122	73,449	375,725	212,474	3,701	3,186
Asilimia ya watahiniwa	11.38	9.48	8.69	44.48	25.15	0.44	0.38

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu kutambua maana ya methali aliyopewa. Asilimia 44.48 ya watahiniwa walichagua D “Nyumba usiyoilala ndani hujui ila yake,” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 212,474 sawa na asilimia 25.15 waliochagua E “Pilipili usiyoila yakuwashia nini” hawakuwa na uelewa wa methali hiyo na walishindwa kutambua kuwa maneno “ya kuwashia nini” yakiwa na maana “usiyaingilie mambo yasiyokuhusu” katika ukamilishaji wa methali hiyo hayana maana sawa na maneno ya methali iliyoulizwa “hujui kunguni wake.” yakiwa na maana kwamba huwezi kukisia uzito wa jambo ambalo halijakufika.

Aidha, watahiniwa 249,667 sawa na asilimia 29.55 walichagua kati ya vipotoshi A “Pema usipopema, ukipema si pema tena” ikiwa na maana pahali pazuri ni pale ambapo hujapafika, B “Kizuri hakikosi ila” ikiwa na maana hakuna kizuri kilichokamilika bila kuwa na kasoro hata kidogo na C “Mtu siri kusema na moyo wake” ikiwa na maana siri huwekwa moyoni kwani ikisemwa sio siri tena. Uchambuzi unaonesha kwamba watahiniwa hao wanaonekana kutokusoma kwa umakini na kuelewa kuwa methali zote hizo zina maana tofauti kabisa na methali iliyoulizwa. Hali hiyo inadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa wa matakwa ya swali. Swali hilo lilitarajiwa kuwa mionganii mwa maswali ambayo watahiniwa wangeweza kuyajibu kwa usahihi kwa kuwa methali hiyo hutumika mara kwa mara katika jamii.

Swali la 27: “Nina mwanangu mweupe nikimtia maji hufa.” Kitendawili hicho kina maana ipi?

- A. Maziwa
- B. Tui la nazi
- C. Majivu
- D. Barafu

E. Karatasi.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D	E*	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	109,407	107,793	159,392	133,366	327,579	3,878	3,338
Asilimia ya watahiniwa	12.95	12.76	18.87	15.79	38.78	0.46	0.4

Swali lililenga katika kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya misemo mbalimbali ya Kiswahili na hasa vitendawili. Asilimia 38.78 ya watahiniwa walichagua jibu E “Karatasi” ambalo ndilo jibu sahihi. Uchaguzi wa vipotoshi A “Maziwa” na D “Barafu” kwa asilimia 12.95 na asilimia 15.79 ambavyo sio majibu sahihi unadhihirisha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa matumizi ya maziwa na barafu hayawezi kuathirika kwa sababu hata kama yanetiwa maji yangeweza kuendelea kutumika. Uteuzi wa kipotoshi C “Majivu” kwa watahiniwa 159,392 sawa na asilimia 18.87 unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kuhusu utambuzi wa rangi ya kijivu ambayo sio nyeupe. Aidha uchaguzi wa kipotoshi B “Tui la nazi” kwa watahiniwa 107,793 sawa na asilimia 12.76 ambacho sio jibu sahihi unaonesha kuwa watahiniwa walishawishiwa na ile dhana ya kuwa na tui la nazi zito yaani lile la mwanzo lakini wakasahau kuwa lipo tui la nazi jepesi ambalo hupatikana kwa kuongeza maji na linatumika tu bila madhara yoyote. Hivyo karatasi ndio jibu sahihi kwa sababu ikiwa bado ina maji haiwezi kutumika na ikilowa zaidi huvurugika kabisa.

Swali la 28: “Bwana mkubwa amelala ndani lakini ndevu zipo nje zapepea.” Jibu sahihi la kitendawili hiki ni lipi?

- A. Ulezzi
- B. Mpunga

- C. Ngano
- D. Mahindi
- E. Mtama.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D*	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	32,459	40,138	33,954	706,152	26,903	2,429	2,718
Asilimia ya watahiniwa	3.84	4.75	4.02	83.59	3.18	0.29	0.32

Swali lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu semi na hasa vitendawili. Hili ni mionganini mwa maswali yaliyojibwa vizuri sana kwani asilimia 83.59 ya watahiniwa waliofanya mtihani walichagua D “Mahindi” ambalo ndilo jibu sahihi. Swali hili lilijibwa vizuri na watahiniwa wengi kwa sababu linaonesha kuwa walikuwa na uelewa wa kitendawili hicho ambacho hutumika mara kwa mara. Asilimia 15.79 ya watahiniwa walichagua katika ya vipotoshi A, B, C na E kwa kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vitendawili na hususan kitendawili walichoulezwa katika swali hili.

Swali la 29: “Kazi mbaya si mchezo mwema.” Methali inayofanana na methali hiyo ni ipi?

- A. Hewala haigombi
- B. Mchezea tope humrukia
- C. Heri kuwa mbichi kuliko kuungua
- D. Hucheka kovu asiyekuwa na jeraha
- E. Hukunyima tongue, hakunyimi neno.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C*	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	64,692	273,929	196,878	179,499	120,354	6,505	2,896
Asilimia ya watahiniwa	7.66	32.43	23.31	21.25	14.25	0.77	0.34

Swali ilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua methali iliyo sawa na “Kazi mbaya si mchezo mwema.” Asilimia 23.31 walichagua jibu sahihi C “Heri kuwa mbichi kuliko kuungua” kuwa methali inayofanana na isemayo “Kazi mbaya si mchezo mwema” ambayo ina maana kwamba ni heri ukaifanya kazi hata kama matokeo yake yakiwa mabaya kuliko kukaa bure na kucheza kwani hakuna mchezo ulio mwema. Asilimia 32.43 ya watahiniwa walichagua kipotoshi B “Mchezea tope humrukia” yenye maana ya aanzishaye ubaya humrudia/huathirika mwenyewe. Uteuzi wa vipotoshi A, D na E unaonesha kwamba watahiniwa husika walikosa ujuzi wa kutambua maana sahihi ya methali hizo hivyo kushindwa kujua ni methali ipi inafanana na ile waliyopewa katika swali.

Swali la 30: Msemo usemao, “kushikwa sikio” una maana ipi?

- A. Kusemwa
- B. Kunong’onezwa
- C. Kuelezwu
- D. Kusengenywa
- E. Kuonywa

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D	E*	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	72,095	484,582	79,651	85,162	115,799	4,412	3,052
Asilimia ya watahiniwa	8.53	57.36	9.43	10.08	13.71	0.52	0.36

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa wa kuchambua misemo mbalimbali na matumizi yake katika mazingira au muktadha. Asilimia 13.71 ya watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kwa kuonesha maana halisi ya msemo “kushikwa sikio” ambayo ni chaguzi E “Kuonywa.” Asilimia 57.36 walichagua kipotoshi B “Kunong’onezwa” jibu ambalo halikuwa sahihi ambalo linaendana na nahau isemayo “kuumwa sikio/kung’atwa sikio.” Waliochagua vipotoshi A, C na D ni asilimia 28.04, watahiniwa hao walishindwa kufafanua maana ya msemo huo kutokana na vipotoshi hivyo vyote kuhusisha taarifa ambayo hutolewa kwa mtu akiwepo au asipokuwepo. Kilichohitajika ili kuweza kujibu swali kwa usahihi ni uelewa wa nahau hiyo.

2.3 Sehemu C: Ufahamu

Katika sehemu hii watahiniwa walitakiwa kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho. Kifungu walichopewa kilisomeka kama ifuatavyo:

Maji ni moja kati ya vitu vitatu muhimu sana vinavyotuwezesha kuishi. Vitu vingine ni hewa na chakula. Hewa ndiyo yenyе umuhimu wa kwanza, ikifuatiwa na chakula. Kusingelikuwa na maji maisha ya binadamu na ya viumbe wengine yasingeliwezekana. Kila mtu anaelewa umuhimu wa maji katika maisha. Maji yanatawala maisha kwa kiasi kikubwa sana. Baadhi ya viumbe kama vile samaki, mamba, kasa, konokono, nyangumi na

wengineo maskani yao ni majini, hivyo maji yakikosekana viumbe hao huweza kuaga dunia.

Binadamu anatumia maji kwa shughuli mbalimbali. Shughuli hizo ni pamoja na kupikia, kufulia, kusafishia vyombo, kuoga na kunywa. Katika sehemu nyingi za nchi yetu watu hutumia maji kwa kumwagilia bustani za mboga, maua na miti. Katika maeneo yenye mito mikubwa na maziwa, maji yake hutumika kwa kumwagilia mashamba kama yale ya mpunga na mahindi. Kilimo cha umwagiliaji kinafaa kwa sababu mkulima anakuwa na uhakika wa kuvuna.

Maji ya mvua huwawezesha watu kulima na kupanda mazao ya chakula na ya biashara. Hivyo zipo sehemu ambazo wakulima hulima kilimo cha umwagiliaji lakini sehemu kubwa ya wakulima hutegemea kilimo cha mvua.

*Kwa ujumla maji yawe ya mvua au yanayotokana na mito au maziwa yana umuhimu mkubwa mno kwa binadamu kama walivyosema wahenga maji ni uhai, hivyo inashauriwa kwamba ni muhimu kwa kila mtu kunywa maji safi na salama ili kulinda **siha** zetu.*

Swali la 31: Vitu vitatu muhimu vinavyomwezesha binadamu kuishi ni vipi?

- A. Hewa, chakula na nyumba
- B. Hewa, maji na chakula
- C. Maji, ushauri na hewa
- D. Maji, hewa na mvua
- E. Chakula, mvua na hewa.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B*	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	56,401	678,082	38,598	34,293	32,064	2,568	2,747
Asilimia ya watahiniwa	6.68	80.27	4.57	4.06	3.8	0.3	0.33

Swali ilikuwa linapima ufahamu wa mtahiniwa baada ya kusoma kifungu cha habari. Swali hili ni miuongoni mwa maswali ya ufahamu yaliyojibowi vizuri kwani asilimia 80.27 ya watahiniwa waliweza kujibu swali kwa usahihi kwa kuchagua vitu vitatu muhimu ambavyo ni B “Hewa, maji na chakula” kutokana na usomaji wa makini, uelewa na uwezo wa kuyatambua mawazo makuu katika habari waliyosoma. Asilimia 6.68 walichagua kipotoshi A “Hewa, chakula na nyumba” kwa vile hawakuwa na uelewa kuwa maji yalikuwa na umuhimu kuliko nyumba. Uchaguzi wa vipotoshi C “Maji, ushauri na hewa”, D “Maji, hewa na mvua” na E “Chakula, mvua na hewa” uliofanywa na watahiniwa 104,955 sawa na asilimia 12.43 unaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa ushauri na mvua haviwezi kuwa na umuhimu zaidi ya maji na chakula kama ilivyoelezwa kwenye habari yenye. Kwa hiyo uchaguzi wa vipotoshi A, C, D na E ulifanywa na watahiniwa amba walishindwa kutambua kuwa vipotoshi hivyo havitoi muhtasari wa mambo matatu muhimu ya habari waliyopewa.

Swali Ia 32: Wakulima wengi kama ilivyoelezwa katika habari hii hulima kilimo kinachotegemea nini?

- A. Mito
- B. Umwagiliaji
- C. Mvua
- D. Mabwawa

E. Maziwa.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C*	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	61,052	247,974	467,394	31,721	30,503	3,345	2,764
Asilimia ya watahiniwa	7.23	29.35	55.33	3.76	3.61	0.4	0.33

Swali hili lilikuwa linapima ufahamu wa mambo muhimu yaliyoelezwa katika habari. Asilimia 55.33 ya watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kwani walichagua jibu C “Mvua” ambalo ndilo jibu sahihi. Asilimia 29.35 walichagua kipotoshi B, “umwagiliaji” kwa kuwa hawakusoma habari kwa makini. Aidha asilimia 14.57 walichagua vipotoshi kati ya A, D na E kwa kuwa walikosa kutambua kuwa “mito,” “mabwawa” na “maziwa” haviwezi kutegemewa katika kilimo kwa sababu kuna maeneo mengi nchini ambayo hayana vyanzo hivyo vya maji.

Swali la 33: Kiumbe yupi kati ya wafuatao halandani na wenzie?

- A. Kima
- B. Mamba
- C. Nyangumi
- D. Kasa
- E. Samaki.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A*	B	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	557,008	58,929	69,940	71,257	80,800	3,723	3,096
Asilimia ya watahiniwa	65.94	6.98	8.28	8.44	9.56	0.44	0.37

Swali ilikuwa linapima ufahamu wa kusoma kwa makini kifungu cha habari na kutambua mambo muhimu yaliyoelezwa. Asilimia 65.94 ya watahiniwa waliofanya mtihani waliweza kujibu swali hili kwa usahihi kwa kuchagua jibu A “Kima” kwa sababu aya ya kwanza ilikuwa inajitosheleza kueleza wanyama wote wanaoishi majini. Watahiniwa waliochagua vipotoshi B, “Mamba” C, “Nyangumi,” D “Kasa” na E, “Samaki” walikuwa asilimia 33.26, watahiniwa hao walikosa ujuzi wa kusoma kwa makini na kupata ufahamu kutoka katika kifungu walichopewa. Aidha watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa katika orodha hiyo ya viumbe ina sifa moja inayofanana ambayo ni kuishi majini isipokuwa Kima ambaye ni jamii ya nyani na tumbili na huishi nchi kavu.

Swali la 34: Kilimo cha umwagiliaji kina sifa gani kubwa?

- A. Uvunaji upo dhahiri
- B. Kinatumia maji ya maziwa makubwa
- C. Kinatumia maji yaliyohifadhiwa
- D. Mazao hayapati magonjwa
- E. Kinalimika majira yoyote.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A*	B	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	269,117	124,299	81,753	75,141	286,743	4,823	2,877
Asilimia ya watahiniwa	31.86	14.71	9.68	8.9	33.94	0.57	0.34

Swali ilikuwa linapima tathmini ya uelewa wa watahiniwa kuhusu habari waliyoisoma. Asilimia 31.86 walijibu swali kwa kuchagua jibu A “Uvunaji upo dhahiri” ambalo ni sahihi. Watahiniwa hao waliweza kuisoma habari na kuelewa kuwa maana ya neno sifa ni uzuri au ubaya wa kitu, hivyo sifa

kubwa ya kilimo cha umwagiliaji ni uvunaji ulio wa uhakika. Asilimia 33.94 ya watahiniwa walichagua kipotoshi E “Kinalimika majira yoyote” ambacho sio jibu sahihi kwa sababu habari hiyo haikueleza kuhusu kilimo kinacholimika majira yote. Uteuzi wa vipotoshi B na C unaonesha kuwa watahiniwa walipotoshwa na dhana ya uhitaji wa maji mengi katika kilimo cha umwagiliaji. Aidha uteuzi wa kipotoshi D unaonesha uelewa mdogo wa usomaji wa habari kwa vile suala la mazao kupata magonjwa halikuelezwa kabisa katika habari waliyopewa.

Swali la 35: Neno “siha” kama ilivyotumika katika kifungu hiki cha habari lina maana gani?

- A. Afya njema
- B. Sifa njema
- C. Maisha mema
- D. Tabia njema
- E. Kinywa safi.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A*	B	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	522,011	96,416	102,676	58,783	60,369	2,027	2,471
Asilimia ya watahiniwa	61.79	11.41	12.15	6.96	7.15	0.24	0.29

Swali lilikuwa linapima maarifa ya watahiniwa kuhusu maana ya misamiati kama ilivyotumika katika kifungu cha habari. Asilimia 61.79 ya watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kutokana na maarifa waliyokuwa nayo na hivyo walichagua jibu A “Afya njema” ambalo ndilo maana sahihi ya neno ‘siha.’ Jumla ya watahiniwa 96,416 sawa na asilimia 11.41 walichagua B “sifa njema” ambalo si jibu sahihi. Inawezekana watahiniwa hao walivutiwa na kipotoshi hicho kwa kuwa kinahusisha uzuri wa kitu na wakahusisha na

neno “siha” ambalo linahusu afya. Aidha, uteuzi wa vipotoshi C “Maisha mema,” D “Tabia njema” na E “Kinywa safi” unaonesha kuwa watahiniwa walikosa maarifa ya kuwawezesha kufahamu maana za misamiati na hasa ikizingatiwa kuwa maneno hayo yanahusiana ingawa yana maana tofauti.

Swali la 36: “Kuaga dunia” ni msemo wenye maana gani?

- A. Kuzirai
- B. Kuzimu
- C. Kulala fofofo
- D. Kufariki
- E. Kufia mbali.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D*	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	32,740	42,344	60,330	677,250	27,632	2,289	2,168
Asilimia ya watahiniwa	3.88	5.01	7.14	80.17	3.27	0.27	0.26

Swali lilikuwa linapima matumizi ya semi za Kiswahili. Swali hili ni mionganii mwa maswali yaliyojibiwa vizuri sana yanayohusiana na maana ya misemo. Asilimia 80.17 walijibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu D “Kufariki” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa hao walikuwa wanajua matumizi sahihi ya nahau hiyo. Watahiniwa 163,046 ambao ni sawa na asilimia 19.30 walichagua kati ya vipotoshi A, B, C, na E ambayo si majibu sahihi kwa kuwa walikosa maarifa kuhusu maana inayowakilishwa na semi za Kiswahili hasa nahau.

Swali la 37: Ni kwanini mtunzi wa habari hii anashauri watu kunywa maji safi na salama?

- A. Ili kuondokana na kiu
- B. Ili kulinda vinywa vyetu
- C. Ili kuburudisha mwili
- D. Ili kuondokana na kichocho
- E. Ili kulinda afya zetu.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D	E*	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	48,792	54,616	49,117	72,858	612,145	4,027	3,198
Asilimia ya watahiniwa	5.78	6.47	5.81	8.62	72.46	0.48	0.38

Swali lilikuwa linapima tathmini ya uelewa wa watahiniwa kuhusu mafunzo yatokanayo na habari waliyosoma. Asilimia 72.46 ya watahiniwa walielewa habari na kuweza kulinganisha ushauri utokanao na habari hiyo kuwa ni E “Ili kulinda afya zetu.” Aidha, kipotoshi A “Ili kuondokana na kiu” kilichochaguliwa na watahiniwa 48,792 sawa na asilimia 5.78 kilionekana kuwashawishi watahiniwa hao wachache kwa sababu watahiniwa hao wameifikiria kiu ya maji zaidi badala ya matokeo yatokanayo na kunywa maji safi na salama. Uteuzi wa vipotoshi B “Ili kulinda vinywa vyetu”, C “Ili kuburudisha mwili” na D “Ili kuondokana na kichocho” ambavyo sio majibu sahihi unaonesha kuwa watahiniwa 176,591 sawa na asilimia 20.9 walikosa uelewa wa maana ya ushauri ambao maana yake ni maelekezo yanayotolewa kwa mtu ili yamsaidie kupata suluhisho fulani. Hivyo vipotoshi hivyo havikuwa ushauri wa kupata suluhisho la kudumu kama lile la kulinda afya zetu.

Swali la 38: Neno “maskani” kama lilivyotumika katika kifungu cha habari lina maana gani?

- A. Nyumba
- B. Makao
- C. Maisha
- D. Mahitaji
- E. Shughuli.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B*	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	193,176	381,999	141,329	60,204	61,284	3,745	3,016
Asilimia ya watahiniwa	22.87	45.22	16.73	7.13	7.25	0.44	0.36

Swali ilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa wa kueleza maana ya msamiati “maskani” kama ulivyotumika katika kifungu cha habari. Asilimia 45.22 walijibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu B “Makao.” Kipotoshi A “nyumba” kilichaguliwa kwa asilimia 22.87 ambayo ni kubwa zaidi kuliko vipotoshi vingine vyote kwa sababu kina mfanano mkubwa na dhana ya neno maskani kwa vile maskani kwa maana nyingine ni mahali anapoishi mtu ambapo huweza kuwa nyumba lakini katika kifungu hiki kinachozungumziwa ni wanyama ambao hawaishi kwenye nyumba ila makao yao ni majini. Uteuzi wa vipotoshi C “Maisha” D “Mahitaji” na E “Shughuli” ambavyo havikuwa majibu sahihi ulifanywa na watahiniwa 262,817 sawa na asilimia 31.11 kutokana na uelewa mdogo wa watahiniwa kuhusu maana ya neno “maskani.”

Swali la 39: Kichwa cha habari kinachofaa kwa kifungu hiki ni kipi?

- A. Hewa ni muhimu
- B. Maji ni uhai

- C. Maji salama
- D. Hewa na chakula
- E. Siha bora.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B*	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	88,750	459,468	83,227	104,644	102,109	3,573	2,982
Asilimia ya watahiniwa	10.51	54.39	9.85	12.39	12.09	0.42	0.35

Swali ilikuwa linawapima watahiniwa kuhusu uelewa wa maudhui ya habari kwa ujumla. Asilimia 54.39 walijibu swali kwa usahihi kwa kubaini kichwa cha habari kuwa ni B “Maji ni uhai.” Watahiniwa 378,730 sawa na asilimia 44.84 waliochagua vipotoshi A, C, D na E walikosa uelewa utokanao na usomaji wa habari kwa makini.

Swali la 40: Methali ipi inaendana na habari hii katika ya zifuatazo?

- A. Mpanda ovyo ndiye mla ovyo
- B. Ahangaikae hupata
- C. Maji hufuata mkondo
- D. Maji yakimwagika hayazoleki
- E. Alisifuye juu limemwangaza.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D	E*	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	177,815	144,645	204,834	205,294	103,698	5,178	3,289
Asilimia ya watahiniwa	21.05	17.12	24.25	24.3	12.28	0.61	0.39

Swali lilikuwa linampima mtahiniwa kuhusu uelewa wa maudhui au ujumbe wa habari kwa ujumla. Asilimia 12.28 walijibu swali kwa usahihi kwa kubaini methali inayoendana na habari waliyoisoma ambayo ni E “Alisifuye juu limemwangaza.” Methali hii ina maana kuwa anayetoa maelezo ya kina kuhusu jambo fulani ni yule anayejua faida za kitu fulani au jambo hilo. Mwandishi wa habari hii anasifu umuhimu wa maji kwa kuwa anajua faida mbalimbali za maji. Asilimia 21.05 ya watahiniwa walichagua kipotoshi A, “Mpanda ovyo ndiye mla ovyo” yenye maana kuwa usipokuwa makini katika kufanya jambo hutopata mafanikio. Uchaguzi huo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuelewa maudhui ya habari waliyoisoma kwani methali hiyo haihusiani kabisa na umuhimu wa maji. Asilimia 17.12 ya watahiniwa walichagua kipotoshi B, “Ahangaikaye hupata” methali yenye maana kuwa mtu anayepata taabu wakati wa kufanya jambo fulani mwishowe hupata mafanikio, maana hii ni tofauti na maudhui ya kifungu cha habari hii. Aidha, asilimia 24.25 walichagua kipotoshi C “Maji hufuata mkondo” ambayo ni methali yenye maana kuwa kila jambo hufuata taratibu na kanuni zake. Hali kadhalika, asilimia 24.3 walichagua kipotoshi D “Maji yakimwagika hayazoleki” methali yenye maana ya kuwa jambo likiharibika halirekebishiki. Kwa ujumla uchambuzi wa swali hili unaonesha wazi kuwa watahiniwa hawana maarifa ya kutosha kuhusu maana za methali kwani methali walizochagua kuwa ni jibu hazihusiani kabisa na kifungu cha habari walichopewa.

2.4 Sehemu D: Ushairi

Katika sehemu hii watahiniwa walitakiwa kusoma shairi lilitolewa na kujibu maswali yanayotokana na shairi hilo.

*Nyumbani kwako kuzuri, japokuwa ni pangoni,
Nyumba yako ni johari, ya mwenzako sitamani,
Hata pawe pa tajiri, hapafai maishani,*

Nyumbani kwako johari, kwingine usitamani.

*Kwingine usitamani, nyumbani kwako johari,
Unaishi kwa amani, na pia kwa ujasiri,
Hiyo kweli abadani, nyumbani kunasetiri,
Nyumbani kwako johari, kwingine usitamani.*

*Uipende nyumba yako, utaona raha yake,
Kisha penda ndugu yako, kwako apaone kwake,
Dunia mahangaiko, usipende pekepeke,
Nyumbani kwako johari, kwingine usitamani.*

*Usichague jirani, bali chagua rafiki,
Usitenge asilani, shauri pia afiki,
Palipo na burudani, kaa nao marafiki,
Nyumbani kwako johari, kwingine usitamani*

Swali la 41: Kichwa cha shairi kinachofaa ni kipi?

- A. Johari ni nyumba
- B. Nyumbani si pangoni
- C. Tuthamini kwetu
- D. Tupende majirani
- E. Tupende marafiki.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C*	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	153,483	194,805	352,715	67,492	68,949	4,275	3,034
Asilimia ya watahiniwa	18.17	23.06	41.75	7.99	8.16	0.51	0.36

Swali lilikuwa linawapima watahiniwa kuhusu uelewa wa maudhui au ujumbe wa shairi kwa ujumla. Asilimia 41.75 walijibu swali kwa usahihi kwa kubaini kichwa cha shairi kuwa ni C “Tuthamini kwetu.” Watahiniwa 484,729 sawa na asilimia 57.38 waliochagua vipotoshi kati ya A, B, D na E walikosa uelewa utokanao na usomaji wa shairi kwa makini.

Swali la 42: Kituo katika shairi hili ni kipi?

- A. Nyumbani kwako johari, kwingine usitamani
- B. Usichague jirani, bali chagua rafiki
- C. Kwingine usitamani, nyumbani kwako johari
- D. Nyumbani kwako kuzuri, japokuwa ni pangoni
- E. Uipende nyumba yako, utaona raha yake.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A*	B	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	581,933	67,427	66,862	62,999	58,749	3,312	3,471
Asilimia ya watahiniwa	68.89	7.98	7.91	7.46	6.95	0.39	0.41

Swali ilikuwa linapima maarifa ya mtahiniwa kuhusu kanuni za utunzi wa shairi. Asilimia 68.89 ya watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu A “Nyumbani kwako johari, kwingine usitamani” kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu utunzi wa mashairi hasa dhana ya kituo. Watahiniwa 256,037 sawa na asilimia 30.3 ya watahiniwa walichagua vipotoshi kati ya B, C, D na E kwa kuwa walikosa ujuzi wa dhana ya kituo ambacho ni mstari wa mwisho unaojirudia katika kila ubeti.

Swali la 43: Neno “johari” kama lilivyotumiwa na mtunzi lina maana gani?

- A. Kitu kilicho dhahiri
- B. Kitu chenye dhamana
- C. Kitu cha thamani
- D. Kitu cha matamanio
- E. Kitu cha kujivunia.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C*	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	92,800	101,570	344,881	123,087	174,594	4,619	3,202
Asilimia ya watahiniwa	10.99	12.02	40.83	14.57	20.67	0.55	0.38

Swali lilikuwa linapima matumizi ya msamiati kama ulivyonumika katika shairi. Asilimia 40.83 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu C “Kitu cha thamani” ambalo ndilo lilikuwa na maana sawa na neno “johari.” Aidha watahiniwa 492,051 sawa na asilimia 58.25 walichagua vipotoshi kati ya A, B, D na E, ambavyo sio majibu sahihi. Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha maana ya neno johari na maneno kama vile “dhahiri” ambalo ni sawa na bayana au waziwazi, “dhamana” lenye maana ya ahadi inayotolewa ili kumdhaminii mtu anayetaka kukopa au anayekabiliwa na mashitaka mahakamani, pia “matamanio” lenye maana ya jambo ambalo mtu anatamani angekuwa nalo. Aidha, neno “kujivunia” lenye maana ya kuringia au hali ya kuona fahari kwa mafanikio yaliyopatikana. Kwa ujumla maneno yaliyomo katika vipotoshi A, B, D na E yana maana ambayo haihusiani kabisa na neno johari.

Swali la 44: Neno “pekepeke” kama lilivyonumiwa na mshairi lina maana gani?

- A. Ukatili
- B. Ufitini
- C. Uonevu
- D. Uchoyo
- E. Uwongo.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B*	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	150,364	193,315	106,530	281,195	105,134	4,977	3,238
Asilimia ya watahiniwa	17.8	22.88	12.61	33.29	12.45	0.59	0.38

Swali lilikuwa linapima matumizi ya misamiati kama ilivyotumika katika habari. Asilimia 22.88 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu B “Ufitini” ambalo ndilo lilikuwa na maana sawa na neno “pekepeke.”

Aidha watahiniwa 643,223 sawa na asilimia 76.15 walichagua vipotoshi kati ya A, C, D na E, kwa kuwa walishindwa kutofautisha hali ya kutokuwa na huruma na udhalimu (ukatili) kumfanyia mtu dhuluma, mateso au unyanyasaji (uonevu), hali ya kutokupenda kutoa kitu (uchoyo) na tabia ya kuwadanganya wengine (uwongo). Hivyo kushindwa kwa watahiniwa hao ni kutokana na kutokuelewa maana mbalimbali za maneno.

Swali la 45: Vina vya kati na vya mwisho katika ubeti wa tatu ni vipi?

- A. Ko na Ke
- B. U na Ke
- C. Du na Ke
- D. Ri na Ni
- E. Ki na Ke.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A*	B	C	D	E	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	489,035	103,262	87,583	107,893	49,382	4,373	3,225
Asilimia ya watahiniwa	57.89	12.22	10.37	12.77	5.85	0.52	0.38

Swali lilikuwa linapima maarifa ya mtahiniwa kuhusu kanuni za utunzi wa shairi. Asilimia 57.89 ya watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu A ‘ko’ na ‘ke’ kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mbinu za utunzi wa mashairi kama vina vya kati na vya mwisho. Asilimia 41.21 ya watahiniwa waliochagua vipotoshi kati ya B, C, D na E walikosa ujuzi wa kuvijua vina vya kati na vya mwisho katika ubeti wa tatu wa shairi hili kwa kuwa hawana ujuzi wa kutosha kuhusu kanuni za utunzi wa mashairi.

Swali la 46: Funzo linalopatikana katika shairi hilo linawakilishwa na methali ipi kati ya zifuatazo?

- A. Raha haiji ila baada ya tabu
- B. Mkataa pema pabaya panamwita
- C. Ukitosa shukuru kupata kuna mungu
- D. Fimbo ya mbali haiui nyoka
- E. Usiache mbachao kwa msala upitao.

Majibu ya watahiniwa

Chaguo	A	B	C	D	E*	Wasiojibu	Mengine
Idadi ya watahiniwa	193,078	218,657	142,832	95,286	185,862	5,178	3,860
Asilimia ya watahiniwa	22.86	25.88	16.91	11.28	22	0.61	0.46

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa kuhusu tathmini ya shairi alilolisoma. Asilimia 22 tu walikuwa na uelewa wa funzo linalopatikana katika shairi, hivyo waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo lilikuwa E “Usiache mbachao kwa msala upitao” methali yenye maana ya usidharau kilicho chako unachodhani kuwa ni kibaya kwa kutegemea kinachopita unachodhani kuwa ni kizuri, shairi hili linahimiza mtu kuthamini kilicho

chake. Watahiniwa waliochagua kipotoshi A “Raha haiji ila baada ya tabu” ni asilimia 22.86, watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kuwa maana ya methali hiyo ni kuwa huwezi kupata raha mpaka usumbuke au utaabike sana, kipotoshi B “Mkataa pema pabaya panamwita” kilichaguliwa na asilimia 25.88, watahiniwa hawa walishindwa kuelewa maana ya methali hiyo ambayo ni anayekataa jambo zuri baya linamngoja. Aidha, kipotoshi C “Ukikosa shukuru kupata kuna mungu” kilichaguliwa na asilimia 16.91, ambayo ni methali yenye maana ya kuwa ukosapo kitu mshukuru mungu kwani ndiye mwenye uwezo wa kutoa, hivyo usiwe na tabia ya kulalamika. Asilimia 11.28 walichagua kipotoshi D, “Fimbo ya mbali haiui nyoka” ambayo ni methali yenye maana kuwa huwezi kufanikisha jambo kwa kutegemea kitu Kilicho mbali nawe. Vipotoshi A–D vina maana ambayo ni tofauti na maudhui ya shairi.

2.5 Sehemu E: Utungaji

Katika sehemu hii, watahiniwa walipewa habari yenye sentensi nne (4) zilizoandikwa bila mtiririko sahihi na walitakiwa wazipange sentensi hizo ili ziwe na mtiririko wenye mantiki kwa kuzipa herufi A, B, C na D.

Swali la 47: Vilevile matunda huongeza damu mwilini.

Swali la 48: Hivyo matunda yana umuhimu mkubwa katika miili yetu.

Swali la 49: Lakini watu wasiokula matunda hupata maradhi kama vile ugonjwa wa fizi, macho na ngozi.

Swali la 50: Kula matunda kunasaidia kuponyesha magonjwa na vidonda haraka, pia husaidia macho kuona vizuri katika mwanga hafifu.

Majibu ya watahiniwa

Swali	Jibu sahihi	Idadi ya watahiniwa	Asimilia ya watahiniwa	% wasiojibu	% mengine	% Jibu E
47	B	347,166	41.1	0.41	0.37	3.52
48	D	300,283	35.55	0.35	0.4	3.39
49	C	295,995	35.04	0.34	0.35	3.78
50	A	513,711	60.81	0.26	0.32	3.8

Swali hili lilitengenye kupima uwezo wa watahiniwa katika upangaji wa mawazo katika mtiririko wenye mantiki. Zaidi ya nusu ya watahiniwa ambao ni asilimia 60.81 waliweza kuandika sentensi ya kwanza kwa usahihi kama ilivyotakiwa. Hata hivyo asilimia ilipungua katika upangaji wa sentensi ya pili kwani ni asilimia 41.1 tu ndiyo walioandika sentensi hiyo kwa usahihi. Katika kukamilisha sentensi mbili za mwisho asilimia ya watahiniwa ilipungua zaidi hadi kufikia asilimia 35.04 kwa sentensi ya tatu na 35.55 kwa sentensi ya nne. Asilimia 3.8 hadi 3.78 walijibu maswali haya kama yale ya kuchagua kwa kujaza kipengele E ambacho hakikuwepo katika sehemu hii ya mtihani. Watahiniwa hawa hawakuelewa maelekezo ya swali na pia inaelekea kuwa walikuwa wanachagua majibu bila kusoma kilichoandikwa kwani wangekuwa wanasoma wangebaini kuwa herufi E haikuwa mionganoni mwa herufi walizopaswa kuziandika katika swali hilo.

3.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa namna watahiniwa walivyojibu maswali unaonesha changamoto mbalimbali ambazo watahiniwa walikumbana nazo walipokuwa wakifanya mtihani. Kwa ujumla kiwango cha ufaulu kwa kila mada kimekuwa ni cha wastani. Uchambuzi unaonesha kuwa katika kila mada kuna maswali yaliyojibwa vibaya na idadi kubwa ya watahiniwa

lakini pia yapo yaliyojibiwa vizuri na Idadi kubwa ya watahiniwa. Kwa upande wa maswali yaliyojibiwa vibaya ni kama vile, swali la 16 kutoka mada ya Sarufi ambapo ni asilimia 19.45 tu ya watahiniwa ndio waliweza kuchagua jibu sahihi. Pia swali la 30 kutoka mada ya Lugha ya Kifasihi lilijibiwa kwa usahihi na asilimia ndogo (13.71). Vile vile ufaulu mdogo ulijitokeza katika swali la 40 lilitotoka katika mada ya Ufahamu, idadi ya watahiniwa waliojibu swali hilo kwa usahihi ni asilima 12.28 tu. Aidha, kwa upande wa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa ni swali la 28 kutoka katika mada ya Lugha ya Kifasihi, ambapo asilimia 83.59 waliweza kuchagua jibu sahihi. Maswali mawili kutoka katika mada ya Ufahamu pia yaliyjibiwa vizuri yaani swali la 31 ambalo lilijibiwa vizuri na asilimia 80.27 na swali la 36 lilitojibiwa vizuri na asilimia 80.17. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa kwa kila mada katika somo la Kiswahili umewasilishwa katika **Kiambatisho A.**

Kutokana na uchambuzi huu, inaonesha wazi kuwa suala la ujifunzaji na ufundishaji wa somo la Kiswahili kwa shule za msingi linatakiwa lifanyike kwa ukamilifu ili kuwawezesha wanafunzi kutumia Kiswahili fasaha. Kwa kuititia wadau mbalimbali wa lugha ya Kiswahili, somo hili linatakiwa kupewa kipaumbele kwa kuwawezesha wanafunzi kupata maarifa ya kutosha kuhusu somo la Kiswahili ili waweze kukabiliana na changamoto mbalimbali za kitaaluma na za kimaisha kuhusiana na lugha ya Kiswahili.

Itambulike wazi kuwa Kiswahili ni lugha ya Taifa, ni sehemu ya utamaduni wa Mtanzania na ni lugha inayotegemewa katika kuziunganisha nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na pia hutumika kimataifa. Hivyo, ni vema juhudu endelevu za kuinua lugha hii zifanyike kuanzia shule za msingi hadi elimu ya juu. Kwa kufanya hivi, lugha hii ya Kiswahili itakuwa imetendewa haki na kupewa hadhi inayostahili katika taifa hili.

4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuwawezesha watahiniwa kupata maarifa na ujuzi wa kutosha na pia katika kuboresha matokeo yao katika mtihani wa Kiswahili mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:

- (a) Mamlaka husika zihakikishe kuwa shule zote za msingi zinakuwa na vitabu vya kiada na vya ziada vya kutosha kwa ajili ya somo la Kiswahili.
- (b) Walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za msingi wanatakiwa kufundisha mada zote kwa ukamilifu kama ilivyoelekezwa katika muhtasari.
- (c) Ili kupata ujifunzaji na ufundishaji wenye mafanikio, walimu wanatakiwa kutoa mazoezi ya kutosha kwa wanafunzi kuhusiana na mada mbalimbali wanazofundisha, ikiwa ni pamoja na kuwapa wanafunzi mrejeo wa matokeo ya mazoezi hayo kila mara.
- (d) Wanafunzi wajengwe kifikra kuhusiana na umuhimu wa somo la Kiswahili katika maisha yao ili waweze kuondoa dhana iliyojengeka kwa wengi ya kuliona somo la Kiswahili kama somo lisilo na tija kwao kwa maisha ya baadaye.
- (e) Wanafunzi wahamasishwe katika kutumia Kiswahili sanifu katika mazungumzo na maandishi yao ya kila siku ili kuboresha misamiati na sarufi ya lugha ya Kiswahili kwa ujumla.

KIAMBATISHO A

**UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA KATIKA
SOMO LA KISWAHILI**

NA	MADA	NAMBA YA SWALI	ASILIMIA YA UFAULU	WASTANI WA UFAULU (%)	MAONI
1.	Sarufi	1	37.62	47.91	Wastani
		2	45.27		
		3	46.67		
		4	50.06		
		5	47.28		
		6	39.99		
		7	77.77		
		8	49.33		
		9	67.64		
		10	32.21		
		11	28.57		
		12	71.56		
		13	64.96		
		14	55.79		
		15	43.91		
		16	19.45		
		17	46.75		
		18	55.69		
		19	28.76		
		20	48.81		
2.	Lugha ya Kifasihi	21	62.9	44.17	Wastani
		22	57.47		
		23	43.63		
		24	48.54		
		25	25.27		
		26	44.48		
		27	38.78		
		28	83.59		
		29	23.31		
		30	13.71		
3.	Ufahamu	31	80.27	55.97	Wastani
		32	55.33		

NA	MADA	NAMBA YA SWALI	ASILIMIA YA UFAULU	WASTANI WA UFAULU (%)	MAONI
		33	65.94		
		34	31.86		
		35	61.79		
		36	80.17		
		37	72.46		
		38	45.22		
		39	54.39		
		40	12.28		
4.	Ushairi	41	41.75	42.37	Wastani
		42	68.89		
		43	40.83		
		44	22.88		
		45	57.89		
		46	22		
5.	Utungaji	47	41.1	43.13	Wastani
		48	35.55		
		49	35.04		
		50	60.81		

